



**BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR**

**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI**

**MKUTANO WA KUMI NA MBILI**

**Kikao cha Nne – Tarehe 18 Septemba, 2023**

**Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi  
na Dua zitasomwa.**

**I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**Ofisi ya Rais Ikulu:**

Hotuba ya Uwasilishaji wa Ripoti ya Ofisi ya Rais Ikulu kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa mwaka 2022/2023.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa Kuhusu Ripoti ya Ofisi ya Rais Ikulu juu ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Ripoti ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa mwaka 2022/2023.

## II. MASWALI:

### Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

80. MHESHIMIWA SULEIMAN HAROUB SULEIMAN (Jimbo la Kiembesamaki) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Baadhi ya vituo vya daladala havipo katika hali nzuri. Miongoni mwa vituo hivyo ni, kituo cha daladala cha Chukwani, Uwanja wa Ndege na vyenginevyo.

Je, Serikali kupitia taasisi husika ina mkakati gani wa kuweka mazingira mazuri katika vituo hivyo.

### Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

26. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Je, Serikali ina mpango wowote ule wa kulitumia eneo la bwawa la maji liliopo Mwanakwerekwe sokoni kwa shughuli za uwekezaji.

### Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

3. MHESHIMIWA MWANAIDI KASSIM MUSSA (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) inawadai madeni ya muda mrefu wafanyabiashara mbali mbali ndani ya mji wa Zanzibar, jambo linalorudisha nyuma jitihada za ukusanyaji wa mapato kwa Mamlaka hiyo.

- (a) Je, Mamlaka ya ZRA ina mikakati ipi ya kuhakikisha inafuatilia madeni hayo ili yaweze kulipwa kwa wakati.
- (b) Je, sababu zipi zinazopelekea kuwepo kwa madeni hayo ya muda mrefu bila ya kudhibitiwa na Mamlaka hiyo.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

69. MHESHIMIWA HAJI SHAABAN WAZIRI (Uzini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Lengo la kuanzishwa kwa Skuli ya Sekondari ya Hasnuu Makame iliyopo Kibuteni, Mkoa wa Kusini Unguja ni kuwa ya Daraja la 1 hadi Daraja la 2.

Je, kwa nini skuli hiyo haikuwa ya Daraja la 3 hadi la 4, wakati katika Mkoa wa Kusini Unguja kuna skuli nyingi za Daraja la 1 hadi Daraja la 2.

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

44. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Je, ni sababu zipi zinazopelekea kuwa na uhaba wa taarifa na makala za uchunguzi (investigative news) kwa vyombo vyetu vya habari vya Serikali.

**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

1. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Katika kuliboresha Soko la Tumbe Baharini, Serikali ilipeleka umeme wa phase tatu (3 Phase) ili uweze kukidhi matumizi bora ya soko hilo. Hata hivyo, inasikitisha kwamba fidia za vipando vya wananchi zilizoruhusu kupitishwa kwa umeme huo zilitolewa na kulipwa kwa wale walioahidiwa fidia na Shirika la Umeme la Zanzibar (ZECO) ilhali wale wa Serikali Kuu hawajafanyiwa malipo yao hadi leo.

- (a) Je, ni watu wangapi na kiasi gani cha fidia kilistahili kulipwa katika upitishaji wa umeme wa phase tatu kuelekea kwenye Soko la Tumbe Baharini.
- (b) Je, kwa nini hadi leo Serikali imeshindwa kuwalipa fidia wananchi walioathiriwa vipando vyao kama ilivyotathmini.
- (c) Je, ni lini Serikali itawalipa fidia zao wananchi waliobakia na kwa utaratibu upi.

III. HOJA ZA SERIKALI:

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Ripoti ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa mwaka 2022/2023.

Ofisi ya Rais Ikulu:

Ripoti ya Ofisi ya Rais Ikulu kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa mwaka 2022/2023.

Zanzibar,  
18 Septemba, 2023.

  
(Raya Issa Msellem)  
KATIBU WA BARAZA.